**JIMBO KATOLIKI KIGOMA**

**CHUO CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI KABANGA**

**S.L.P 42, KASULU, KIGOMA.**

**REG/HAS/023 (FBO)**

**Email**: admission@kcohas.or.tz

**Website**: www.kcohas.or.tz

**Mobile:** 0755785928, 0762 43 77 80, 0765032756 and 0739 909 165, 0621,577,964

# FOMU YA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UUGUZI NA UKUNGA (NURSING AND MIDWIFERY) SEPTEMBER 2025/2026

Kwa: ………...............................

Unataarifiwa kuwa umechaguliwa kujiunga na taasisi ya mafunzo ya afya Kabanga kwa kozi ya Uuguzi na Ukunga **(Ordinary Diploma in Nursing and Midwifery)**

**Tarehe ya kuripoti ni 04/10/2025 , mwisho wa kuripoti ni tarehe 26/10/2025**

Hapa tumeambatanisha yafuatayo:

1. Fomu ya kujiunga na chuo
2. Sheria za chuo ambazo wewe mwenyewe na mzazi/mlezi anapaswa kuzisoma, kuzielewa na kisha kuweka sahihi ikimaanisha unazikubali.
3. Fomu ya ada na namna ya kulipa.

**MAHITAJI**

1. Cheti cha kuthibitisha afya ( Medical certificate form)
2. Kurejesha nakala ya kukubali sheria za chuo
3. Ada na michango mbalimbali kama ilivyo ainishwa katika muundo wa ada hapo chini.
4. Cheti halisi cha kidato cha nne **(4 )NA SIYO COPY**
5. **Kitambulisho cha taifa (NIDA)** Ni muhimu kwa ajili ya kutengeneza bima ya afya
6. Cheti cha kuzaliwa
7. Malipo yote yaliyo orodheshwa yapitie **BENKI** kupitia akaunti ya **KABANGA NURSES AND MIDWIVES TRAINING SCHOOL ACCOUNT NO. 51403500108 NMB.**
8. Ada ya mwaka ni Shilingi milioni moja na laki sita elfu tu (**1,600,000.00) fedha hizi zitalipa kwa awamu nne**
9. Mahitaji mengine ya mwanafunzi kwa mwaka ni shilingi laki saba na elfu sitini (**760,000.00**). Fedha hizi zinaweza kulipwa kwa awamu tatu (3) au kwa mkupuo kama ilivyofafanuliwa kwenye jedwali ukurasa wa mwisho .
10. Mwanafunzi atapokelewa chuoni baada ya kulipa malipo ya kwanza ya ada ambayo ni shilling laki sita **(600,000,** na shilingi laki nne (**400,000)** ambayo ni michango mingine, jumla inakuwa shilingi milioni moja tu **(1,000,000 tu)**

**Ifuatayo ni orodha ya mahitaji ya mwanafunzi anapofika chuoni:**

**1.** Viatu vyeusi vya ngozi visivyo kuwa na mwinuko hususani kwenye kisigino na soksi nyeupe

2. Kwa mwanafunzi atakayehitaji sweta liwe rangi nyeupe

3. Mashuka mawili rangi ya

    i. Blue bahari kwa wavulana

    ii. Pinki kwa wasichana

4. Chandarua

5. Ndoo kwa ajili ya kuogea

6. Karatasi ream tatu (3) (**dobble A)**

7. Nguo za michezo

8. Saa ya mkononi yenye mshale wa sekunde **- lazima**

9. Kadi ya bima ya afya ( iwapo unayo)

1. Vifaa vya kujifunzia chuoni na wodini vinapatikana chuoni kwa gharama ya shilingi **100,000/=** au unaweza kununua mwenyewe kwa kuzingatia ubora na maelekezo yake.


    i. Blood pressure machine 1 – (**Mannual na siyo digital)**

    ii. Stethoscope 1

    iii. Thermometer 1 **Mannual na siyo digital**

    iv. File

    v. Tape measure






**JUMANNE A. BALUHYA**

**MKUU WA CHUO**

**JIMBO KATOLIKI LA KIGOMA**

**TAASISI YA MAFUNZO YA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI KABANGA**

**SHERIA ZA CHUO KWA MAELEKEZO YA WIZARA YA AFYA**

1. Mwanafunzi ataheshimu tarehe ya kuwasili chuoni baada ya likizo yake.Hatua za kinidhamu zitachukuliwa kwa mwanafunzi yeyote atakaye chelewa
2. Mwanafunzi akiwa chuoni atatakiwa kula chakula kinacho tolewa na chuo.
   Hakuna ruhusa kwa mwanafunzi yeyote kujipikia chakula. Kama atakuwa na sababu maalumu ya kufanya hivyo atapewa kibali maalumu kutoka kwa mkuu wa chuo baada ya kujadiliwa na kamati ya nidhamu ya chuo cha afya na sayansi shirikishi kabanga.
3. Mwanafunzi awapo maeneo ya hospitali anatakiwa kuwa amevaa sare ya chuo, hata kama hatakuwa kazini (mfano anaposalimu /kuona wagonjwa) Akionekana kinyume cha utaratibu tajwa atawajibishwa na mtumishi yeyote wa hospitali au chuo.
4. Mwanafunzi akiwa mgonjwa analazimika kupata matibabu ndani ya hospitali. Hairuhusiwi kwa mwanafunzi yeyote kutumia dawa alizojinunulia bila maandishi kutoka kwa mganga au daktari. Siku za mapumziko kwa ajili ya ugonjwa zitaandikwa na daktari. Mwanafunzi atamuonyesha mwalimu / wadeni au mkuu wa wodi siku alizopewa kwa ajili ya mapumziko ya ugonjwa.
5. Wanafunzi wote wanatakiwa kuvaa mavazi ya heshima muda wote wawapo chuoni na nje ya chuo. **Suruali zinazobana, fupi na jeans haziruhusiwi.** Pia utunzaji wa nywele ni muhimu, Kusuka nywele tano au kunyoa ndiko kunako ruhusiwa. Usukaji na unyoaji usiokuwa wa nidhamu (Panki) kusuka au kuweka dawa, rasta kichwani na kunyoa kipara hakuruhusiwi, Mwanafunzi anatakiwa ***kuwa na nywele fupi***. Nguo zenye picha na maandishi yasiyohusiana na maadili hayaruhusiwi.
6. Mafunzo ya mwanafunzi yamegawanyika katika sehemu kuu mbili: mafunzo ya darasani na wodini. Sehemu zote mbili zina umuhimu sawa. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuheshimu mpangilio wa kazi chuoni na wodini kadri atakavyo kuwa amepangiwa na wakuu wake. Hairuhusiwi mwanafunzi kubadilisha zamu yake bila ruhusa toka kwa mkuu wake wa eneo au kitengo.
7. Wanafunzi wawapo wodini na hostel hawaruhusiwi kuongea kwa sauti kubwa inayowasumbua wagonjwa na watu wengine.
8. Muda wa mwisho wa kuingia katika eneo la hospitali na chuo ni saa 12.30 jioni. Kwa sababu ya mazingira ya huku. Mwanafunzi ataruhusiwa kwenda nje ya mazingira ya Hospitali na chuo sio zaidi ya km nane (8.) Siku za Jumamosi, Jumapili na Sikukuu. Kama kutakuwa na sababu maalumu za kwenda nje zaidi ya siku zilizo tajwa hapo juu atatakiwa kuomba ruhusa kwa maandishi. Majina yote ya wanafunzi walio nje ya chuo yataandikwa kwenye daftari na kuainisha sababu za kuwa nje yachuo. Mwanafunzi atakayeingia Hospitalini na chuo bila taarfa na sababu maalum baada ya muda uliotajwa hapo juu atawajibishwa.
9. Mwanafunzi akilala nje ya chuo bila sababu, kibali au ruhusa maalumu atakuwa **amejifukuzisha chuo.**
10. Upigaji wa vyombo vya muziki katika eneo la hospitali na chuo hauruhusiwi. Siku za sikukuu na sherehe mwisho wa kupiga mziki utakuwa saa 4.00 (nne kamili) usiku. Mziki huo utatakiwa kuwa na sauti ndogo/ ya kawaida
11. Mwanafunzi haruhusiwi kutumia simu akiwa darasani na wodini. Simu zote ziachwe chuoni ( bwenini) wakati mwanafunzi anapokuwa darasani ama wodini

12. Hakuna wageni wa wanafunzi watakao ruhusiwa kuingia chuoni wakati wa muda wa vipindi au siku za kazi. Wageni wote wanaruhusiwa kuwatembelea wanafunzi siku za Jumamosi, Jumapili na siku za sikukuu kuanzia saa 7.00 (Saba) mchana. Mwisho wa wageni kuwepo eneo la chuo ni saa 12.00 jioni.
13. Mwanafunzi hataruhusiwa kumtunza ndugu yake akiwa amelazwa hospitalini kama itahitajika kufanya hivyo lazima ruhusa itoke kwa mkuu wa chuo kwa sababu maalumu.
14. Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia swala zima la usafi wa mazingira ya chuo na hospitali.
15. Mwanafunzi akihusika na uharibifu wa mali ya chuo au hospitali, atatakiwa kurudisha gharama au kununua kifaa kilicho haribika.
16. Wanafunzi wote wanatakiwa kuhudhuria eneo la sala na kusali kila siku saa moja na robo asubuhi kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa na kushiriki shughuli mba mbali mfano: kuandaa somo la kitaaluma na kuwasilisha kwa wanafunzi na waalimu Utaratibu huu utafuatwa na wanafunzi wote watakao kuwa katika chuo hiki.
17. Mwanafunzi awapo chuoni atatakiwa kujihusisha na michezo kama sehemu ya mafunzo. Ratiba ya michezo itafuatwa kama ilivyoratiba nyingine ndani ya chuo hiki.
18. Taarifa zozote zile za kifamilia zinazomhusu mwanafunzi hasa zile zinazohusiana na magonjwa ama kifo lazima zipelekwe ofisi ya mlezi ( wadeni) wa wanafunzi) au ofisi ya mwalimu kwa mawasiliano na siyo kumpa mwanafunzi. Mwanafunzi hatasikilizwa endapo taarifa hizo zitamfikia yeye /atatoa mwenyewe ofisi ya mwalimu
19. ***Mwanafunzi atakaye jihusisha na wizi wa mali ya chuo, hospitali, na ya mwanafunzi mwenzake atafukuzwa shule mara moja***

Taratibu nyingine zinapatikana kwenye sheria zilizowekwa na wizara ya afya, Idara ya Mafunzo ya Vyuo. Mwanafunzi atasomewa na kupewa sheria hizo afikapo chuoni. Mzazi/mlezi unatakiwa kusoma sheria hizi na kuweka saini.

**FOMU YA KUKUBALI SHERIA ZA CHUO.**

Fomu hi iijazwe na mzazi/mlezi/ mwajiri wa mwanafunzi na irudishwe chuoni wakati mwanafunzi anapo ripoti.

1. Mimi (mzazi/mlezi/ mwajiri) ……………………………………………………………….

   Nimesoma na kuelewa sheria za chuo cha afya na sayansi shirikishi – Kabanga. Nakubaliana na sheria hizo na niko tayari kuwa kijana wangu awajibishwe ikiwa atakiuka utaratibu huo.

   Saini ya Mzazi / Mlezi/ mwajiri ………..........……Tarehe……………………………

2. Mimi (Mwanafunzi) ………………………………………………………………. Nimesoma na nimeelewa sheria za taasisi ya afya na sayansi shirikishi Kabanga. Niko tayari kuwajibishwa ikiwa nitakiuka utaratibu huo.

   Saini ya mwanafunzi ………………….......…..Tarehe……………………………………..

   Tunaomba uthibitishe kama wewe/mwanao atakuja chuoni. Usipofanya hivyo nafasi yako/yake itachukuliwa na mwingine.

   Tuthibitishie kwa kupiga simu / email tajwa hapo juu, au unaweza kurudisha fomu.

   Mimi (mwanafunzi) ..........................................................................................

   Ninaahidi nitakuja chuoni tarehe tajwa naomba kutunziwa nafasi yangu.

   Saini ya mwanafunzi/mlezi/mwajiri ........................................................................

**KABANGA COLLEGE OF HEALTH AND ALLIED SCIENCES P.O.BOX 42 KASULU**

**REG/HAS/023 (FBO)**

**MEDICAL EXAMINATION FORM:**

Candidate Name ………………………………………………………………………..

Home address..………………………………………………………………………

Please examine the followings: **Findings**

1. ESR ……………………………………….....
2. Hb …………………………………………
3. Stool …………………………………………
4. Urine ………………………………………….
5. Full physical Examination …………………………………….......
6. Vision ………………………………………...
7. Hearing …………………………………….....
8. B/P …………………………………………....
9. Lungs …………………………………………....
10. Others …………………………………….......
11. Previous chronic diseases eg Asthma, Heart diseases, Allergy, Psychosis..............
12. Pregnancy Test for female students................... ……………………...

________________________________

**Signature of the examining Doctor and Official stamp**.

**JIMBO KATOLIKI KIGOMA**
**KABANGA CHUO CHA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI - KASULU**
**MUUNDO WA ULIPAJI WA ADA KWA KOZI YA UUGUZI NA UKUNGA MWAKA 2025/2026**

| S/N | UFAFANUZI/MAELEKEZO | NGAZI YA 4 | NGAZI YA 5 | NGAZI YA SITA 6 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | ADA | 1,600,000 | 1,600,000 | 1,600,000 |
| | **JUMLA** | **1,600,000** | **1,600,000** | **1,600,000** |
| **Ada tajwa yaweza kulipwa kwa awamu nne (4) au mkupuo mmoja** | | | | |
| **AWAMU ZA ULIPAJI** | | | | |
| | 1. AWAMU YA KWANZA ANAPO RIPOTI CHUONI | 600,000 | 600,000 | 600,000 |
| | 2. AWAMU YA PILI - JANUARY | 400,000 | 400,000 | 400,000 |
| | 3. AWAMU YA TATU - APRIL | 300,000 | 300,000 | 300,000 |
| | 4. AWAMU YA NNE - JULAI | 300,000 | 300,000 | 300,000 |
| | **JUMLA KUU** | **1,600,000** | **1,600,000** | **1,600,000** |
| | **GHARAMA ZA MWANAFUNZI** | | | |
| 2 | MALAZI | **BURE** | **BURE** | **BURE** |
| 3 | USAJILI | 50,000 | - | - |
| 4 | MITIHANI YA NDANI | 300,000 | 300,000 | 300,000 |
| 5 | MCHANGO VIFAA VYA MAZOEZI WODINI | 200,000 | 200,000 | 200,000 |
| 10 | TEHAMA (INTERNET) | 60,000 | 60,000 | 60,000 |
| 11 | GHARAMA ZA MACHAPISHO | 100,000 | 100,000 | 100,000 |
| 12 | FEDHA YA UKARABATI | 50,000 | 50,000 | 50,000 |
| 13 | CHETI CHA KUHITIMU | - | - | 10,000 |
| | **TOTAL** | **760,000** | **710,000** | **720,000** |
| | **FEDHA HIZI ZITALIPWA KWA AWAMU TATU (3)** | | | |
| | 1. AWAMU YA KWANZA ANAPORIPOTI | 400,000 | 400,000 | 400,000 |
| | 2 .AWAMU YA PILI MWEZI – JANUARY | 180,000 | 155,000 | 160,000 |
| | 2. AWAMU YA TATU - APRIL | 180,000 | 155,000 | 160,000 |
| | **JUMLA KUU** | **760,000** | **710,000** | **720,000** |

**FEDHA HIZI ZILIPWE KUPITIA AKAUNTI NAMBA NMB 51403500108**

**NB: Mwanafunzi hataruhusiwa kuendelea na masomo kama hatakuwa amelipa ada na michango kwa wakati.**

**NB:**

1. ADA YA MITIHANI YA WIZARA 150,000 ITALIPWA MUHULA WA PILI
2. ADA YA UDHIBITI UBORA(NACTEVET) 20,000 INALIPWA MWANZO WA MWAKA WA MASOMO
3. BIMA YA AFYA – NHIF 50,400 INALIPWA KILA MWAKA
4. Chakula kinapatikana kantini ya chuo kati ya gharama ya kuanzia shilingi 1,000-3000 kwa kifungua kinywa na shilingi 1,000 – 4,000 kwa chakula cha mchana na jioni

**GHARAMA ZA NYONGEZA (GHARAMA ZA MWANAFUNZI)**

**Fedha hizi zinalipwa moja kwa moja chuoni kwa mhasibu wa chuo**

| No | UFAFANUZI/MAELEKEZO | NGAZI YA 4 | NGAZI YA 5 | NGAZI YA 6 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mazoezi ya Afya ya jamii | - | 200,000 | - |
| 2 | Utafiti | - | - | 100,000 |
| 3 | Mazoezi ya afya ya akili | - | - | 200.000 |
| 4 | Usajili baraza la uuguzi Tz (TNMC) | 30,000 | - | - |
| 5 | Kitambulisho | 10,000 | - | - |
| 6 | Kitabu cha mazoezi ya vitendo | 15,000 | 53,000 | - |
| 7 | Mchango wa umoja wa wanafunzi | 20,000 | 20,000 | 20,000 |
| 8 | Sare za mwanafunzi | 90,000 | - | - |
| | | **165,000** | **273,000** | **320,000** |
| | | | | |

**NB: FEDHA YA MAZOEZI YA AFYA YA JAMII NA AFYA YA AKILI ITALIPWA MUHULA WA PILI WA MASOMO.**

**FEDHA HII ITALIPWA MOJA KWA MOJA KWA MHASIBU WA CHUO NA KUPEWA RISITI.**

**JUMANNE A. BALUHYA**

**MKUU WA CHUO**

THE PRINCIPAL
(KACOHAS)
P.O.Box 42 KASULU
KABANGA COLLEGE OF HEALTH & ALLIED SCIENCES